

ASb
approved



Mkoba Uzungumzao

Mutugi Kamundi

Wiehan de Jager

Kiswahili

African
Storybook.org




Hapo zamani za kale aliishi jitu jike lililoitwa Motio. Siku moja lilipokuwa likitembea kando mwa ziwa liliwaona wasichana watatu, Lisa, Vera na Elsa. Likawauliza, "Ni nani kati yenu anayependwa na wazazi wote wawili?"



Lisa alijibu kwanza, akasema, "Mamangu hunipenda zaidi."
Vera naye akasema, "Babangu hunipenda zaidi." Elsa
akasema, "Baba na mama wanipenda sawa."



Motio alimwambia Elsa amfuate akamsaidie kuliinua tita la kuni amwekee mgongoni. Elsa alimfuata Motio bila kuogopa.



Walipotembea hatua chache, Elsa alimwuliza Motio, "Zi wapi kuni zako nikusaidie?" Motio akajibu, "Ziko karibu na ile miti."



Walipofika hapo, Elsa akamwuliza Motio tena, "Zi wapi kuni zako?" Motio akajibu, "Haziko mbali kutoka hapa."



Walipokuwa wakitembea, walikutana na mwanamume.
Mwanamume huyo alimwuliza Motio, "Mtoto wako
anaitwaje?" Motio akajibu, "Anaitwa Mkoba Uzungumzao."



Elsa aliimba kwa sauti, "Mimi kamwe si mkoba. Mkoba hauongei. Ninaitwa Elsa. Lo! Nyumbani kwetu, Mama nimpendaye, Baba nimpendaye, Kata nilinywealo maziwa."



Mwanamume huyo alipousikia wimbo wa Elsa, alimhurumia, akamwuliza amwelezee juu ya wazazi wake. Alimnusuru kutoka kwa Motio na kumrudisha kwa babake na mamake. Wazazi wake walimshukuru mwanamume huyo na wakaishi kwa furaha na mtoto wao.

You are free to download, copy, translate or adapt this story
and use the illustrations as long as you attribute in the
following way: Caroline Lentupuru Author - Caroline

Lentupuru

Translation - Mutugi Kamundi

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - Longer paragraphs © African Storybook Initiative

2014

Creative Commons: Attribution 3.0

Source www.africanstorybook.org



